

## MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA



**TAARIFA KWA UMMA**

**11 Juni, 2018**

### **KUONDOA KATAZO LA UINGIZAJI NCHINI WA NYAMA NA BIDHAA ZA NYAMA KUTOKA NCHINI AFRIKA KUSINI LILILOWEKWA KUFUATIA MLIPUKO WA UGONJWA WA “*LISTERIOSIS*”**

1. Mnamo tarehe 7 Machi, 2018 Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) iliweka katazo la uingizaji nchini wa nyama na bidhaa za nyama kutoka nchini Afrika Kusini. Katazo hilo lilitokana na mlipuko wa ugonjwa wa *Listeriosis* uliotokea nchini humo ambao ulisababishwa na ulaji wa bidhaa za nyama zilizochafuliwa na bakteria aina ya *Listeria monocytogenes*.
2. Sanjari na usitishwaji uliofanyika, TFDA kupitia mifumo yake ya udhibiti wa usalama na ubora wa chakula ilichukua hatua zaidi ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi ili kubaini endapo bidhaa zilizohusishwa na mlipuko huo ziko katika soko. Vilevile, TFDA ilichukua sampuli za bidhaa za nyama katika soko na kuzifanyia uchunguzi wa kimaabara ili kujiridhisha kama hazina uchafuzi wa bakteria wanaosababisha ugonjwa wa *Listeriosis*.
3. Ukaguzi uliofanyika ulibaini kuwa bidhaa zilizosababisha mlipuko wa *Listeriosis* katika nchi ya Afrika Kusini hazikuingizwa katika soko la Tanzania. Hali kadhalika, sampuli za bidhaa zilizofanyiwa uchunguzi wa kimaabara hazikuwa na uchafuzi wa bakteria wanaosababisha ugonjwa wa *Listeriosis*.
4. Vilevile, TFDA imepokea taarifa kuhusu hatua zilizochukuliwa na Mamlaka za udhibiti za nchini Afrika Kusini katika kukabiliana na mlipuko uliotokea na kujiridhisha kwamba kwa sasa bidhaa za nyama zinazouzwa nchini humo na zile zinazosafirishwa kwenye nchi nyingine ni salama.
5. Hivyo basi, TFDA inaondoa katazo la kuzuia uingizaji wa nyama na bidhaa za nyama kutoka Afrika Kusini lililokuwa limetolewa tarehe 7 Machi, 2018. Hata hivyo, bidhaa za nyama kutoka viwanda vya Enterprise Foods Polokwane (ZA 33), Enterprise Foods Germiston (ZA 126) na RCL Foods Consumer – Chicken (ZA 32) ambavyo vilizalisha bidhaa zilizohusishwa na mlipuko wa *Listeriosis* zinaendelea kuzuiwa kuingizwa nchini.
6. Aidha, waingizaji wa nyama na bidhaa za nyama nchini wanakumbushwa kuendelea kuzingatia taratibu za uingizaji wa bidhaa hizo nchini ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanapata vibali vyote vinavyohitajika.
7. TFDA kupitia mifumo yake ya udhibiti itaendelea kusimamia kwa umakini mkubwa uingizaji wa bidhaa za chakula nchini zikiwemo nyama na bidhaa za nyama na kufanya ufuatiliaji maalum katika soko na kufanya uchunguzi wa kimaabara wa nyama, bidhaa za nyama pamoja na bidhaa nyingine zote zenye uwezekano wa kuchafuliwa na bakteria wanaosababisha ugonjwa wa *Listeriosis* ili kulinda afya ya jamii.

**Imetolewa na:**

**Kaimu, Mkurugenzi Mkuu  
Mamlaka ya Chakula na Dawa  
S.L.P 77150, Dar es Salaam  
[www.tfda.go.tz](http://www.tfda.go.tz)  
Piga simu bila malipo: 0800110084**